

LBE 2009 – Migration

Episode 9: Return to Mali

Author: Mahamadou Koné

Editor: Thomas Mösch

Translator: Anne Thomas

Characters:

Scene 1:

Narrator (Male or female)

Mamadou Diaby, 31

Scene 2:

Narrator

Daouda Tounkara, age ?

Intro:

Hujambo na karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu Uhamiaji kati ya Afrika na Ulaya. Kwa Waafrika wengi Ulaya ni peponi. Vijana wengi wa Kiafrika hujaribu kukimbilia Ulaya, kwa lengo la kuhepa ukosefu wa kazi na shida za makwao. Wako tayari kufanya lolote: wengine huwa wahamiaji wasio halali baada ya viza zao za utalii katika nchi za Ulaya kumalizika, wengine wanahatarisha maisha yao kwa kudandia mashua ili kufika pwani za nchi za Ulaya kupitia baharini. Mamadou Diaby na Daouda Tounkara ni vijana wawili kutoka Mali ambao walichagua njia ya kwanza. Lakini walivunjika moyo baada ya kuishi miaka michache hapa Ulaya na wakaamua kurudi nyumbani.

Scene 1:

1. SFX: Customer reception

2. Narrator:

Tuko mji mkuu wa Mali, Bamako, katika duka la kutengenezea fanicha la Mamadou Diaby, liko katikati kwenye eneo kubwa la kufanyia biashara mjini. Mamadou amekaa kwenye Kompyuta yake – nyuma yake televisheni imewashwa – anaonekana kuwa ni mtu mwenye furaha. Miaka michache iliyopita, hakudhani kama angekuwa na hali aliyonayo sasa...Kijana huyu anatoka kwenye kabila la Soninke huko nchini Mali, watu wanaopenda kusafiri. Akiwa na miaka 23, aliamua kwenda Ufaransa na kupanga kutafuta utajiri. Miaka michache kabla ya hapo alikuwa ameacha masomo na kuanzisha biashara ndogo katika mji wa Bamako. Mnamo mwaka 2001, aliwasili Paris – ilikuwa ni mara yake ya kwanza kusafiri nje ya nchi yake Mali. Hakuweza kusahau hilo kamwe:

3. O-Ton Mamadou, French :

"Huwa ni vugumu; ni kama vile kwenda kwenye dunia nyingine. Mali na Ufaransa , au Ulaya, haziko sawa. Kuna tofauti kubwa . Ilikuwa ni mara yangu ya kwanza kusafiri. Mara ya kwanza kwenda Ulaya."

4. Narrator:

Alipofika Ulaya kwa visa ya utalii ya miezi mitatu, kijana huyo baadaye aliamua kuendelea kukaa – kinyume cha sheria. Halafu ilibidi akabiliane na ukweli mgumu hasa katika kutafuta kazi:

5. O-Ton Mamadou, French:

"Kila mmoja anafamu kuwa sio rahisi kupata kazi nchini Ufaransa. Huwezi kufanya kazi kama hauna makaratasi. Lazima uwe na kibali cha kuishi ndipo uwe na ruhusa ya kufanya kazi. Mimi sikuwa na kibali hicho. Kwa hivyo sikuwa na budi ila kufanya kazi kimagendo tu – hutokea hivyo iwapo huna makaratasi ya kuishi."

6. Narrator:

Wahamiaji haramu hawawezi kupata msaada kutoka kwenye mashirika ya kiserikali yanayosaidia kuwatafutia watu nafasi za kazi. Watu hao hawatambuliwi na serikali za mitaa kwa hivyo hawana haki ya kupewa misaada. Inawabidi wafanye kazi kinyume cha sheria – mara nyingi wanaishia kusafisha mikahawa midogo midogo, kufagia barabara, kuwa vinyozi na kadhalika. Hawalipwi ujira mzuri. Mara nyingi wananyanyaswa na waajiri wao, ambao hufaidika kwa ajili ya hali yao. Wahamiaji wasio halali huwa wanafikiria kuwa ni wajibu wao kukubali kila wanalotendewa. Hawapingi au hawalalamiki kwa sababu wanaogopa kujihusisha na maswala ya polisi. Hii inaweza kusababisha warudishwe kwao. Wahamiaji mara nyingi huwa wanakamatwa kwenye misako ya polisi. Mamadou alibahatika. Aliweza kuishi nchini Ufaransa bila kibali kwa miaka saba. Lakini mwishowe hakuweza kuvumilia tena. Alihisi kuwa ananyanyaswa na waajiri wake, ambao walitumia kigezo cha yeye kutokuwa na kibali cha kuishi, na wakati wote alikuwa anahofia kukamatwa na polisi. Mwishoni mwa mwaka 2007, alirudi Mali.

7. SFX: in the shop

8. Narrator:

Mamadou amefungua duka la fanicha katika mji wa Bamako, alitumia fedha alizokuwa ameziweka. Anatuonyesha:

9. O-Ton Mamadou, French: Guided tour

"Hivi ni vitanda, kutoka China, Dubai na Uturuki. Hizi hapa ni meza za kompyuta kutoka China. Hii ni fanicha ya chumba cha kulia chakula kutoka Dubai. Na zile pale ni meza, viti vya ofisi na rafu za kuwekea vitabu."

10. Narrator:

Kwa sasa Mamadou hana majuto. Ana mikataba na mashirika ya umma pamoja na ya kibinafsi. Anasafiri sana kwa ajili ya kazi yake:

11. O-Ton Mamadou, French :

"Ninanunua bidhaa zangu kutoka Ulaya na Asia. Ninasafiri kwenda Dubai, China, na Uturuki kwa ajili ya kununua bidhaa ambazo naziuza hapa Mali. Hata ikiwezekana niende Ufaransa siwezi kukaa huko. Labda ninaweza kwenda huko kutembea. Mnaona shughuli zangu sasa. Siwezi kuacha haya yote na kwenda kuhangaika Ufaransa."

12. Narrator:

Kwa vile ameshakaa Ulaya na Afrika, Mamadou anahisi anaweza kufananisha sehemu hizo mbili:

13. O-Ton Mamadou , French :

"Mimi ninaishi vizuri kuliko Wamali walioko Ufaransa. Sisemi kuwa nina maisha mazuri kuliko Wamali wote wanaoishi

Ufaransa lakini wengi wao wanapata taabu, wana maisha magumu."

14. Narrator:

Mamadou ana miaka 31 tu lakini tayari yeye ni mkurugenzi mkuu. Amewaajiri wafanyakazi sita. Anasema vijana lazima wawe na macho ya kuona mbali:

15. O-Ton Mamadou, French :

"Inasikitisha kuwaona vijana wa miaka 15, 16, 19, 20 ambao wanataka kwenda Uhispania, Italia kwa kujitumbukiza baharini, wanapanda mashua ambazo baadaye zinazama. Kuna watu wengi ambao hufa kwa kujaribu kwenda Ulaya. Maisha sio lazima yawe mazuri kule. Tulikuwa Ulaya, tunajua ukweli wa mambo."

16. Narrator:

Mamadou anasema kuna nafasi tele barani Afrika. Bara hilo linawahitaji watoto wake kuleta maendeleo:

17. O-Ton Mamadou, French :

"Ningependa Wamali wote walioko nje, Waafrika wote walioko Ulaya, Asia, na kila mahali ulimwenguni, warudi nyumbani wakafanye kitu huko. Sio lazima wote wafanye biashara kama yangu ya fanicha. Kuna mambo mengi ya kufanya."

Scene 2:

18. O-Ton Daouda beneath Fakoly's music, French :
« Hiki ni kipande cha muziki nilichokitengeneza na Fakoly
Doumbia, mwanamuziki kutoka Mali....
(fade out under following text)

19. Narrator:

Daouda Tounkara ni kijana mwingine kutoka Mali ambaye alikuwa na ndoto ya kuufuma utajiri kutoka Ulaya. Sawa na Mamadou, aliacha shule na kwenda Ufaransa, na baadaye akarudi Mali kujenga maisha yake. Tulimtembelea kwenye studio yake ya kutengeneza filamu katika eneo maarufu mjini Bamako. Ndani ya studio hiyo kuna Kompyuta kadhaa na vifaa vya kufanyia uhariri. Pia kuna Kamera kadhaa. Je. Mhamiaji huyu wa zamani amepataje vifaa hivi vyote?

20. SFX : Music Fakoly

21. Narrator :

Mwezi Januari mwaka 2002, Daouda alikwenda Paris. Alipanga kukaa kwa muda mrefu sana hata ingawa visa yake ilikuwa ya utalii tu. Lakini hakuchelewa kuuona ukweli wa mambo:

22. O-Ton Daouda, French :

"Haikuwa rahisi huko Ufaransa. Nilikaa miezi saba bila kupata kazi. Nilivunjika moyo, lakini nilipambana na mwishowe nilibakia Ulaya kwa miaka kama mitano hivi."

23. Narrator:

Alifanya kazi ambazo hangekubali kuzifanya nchini Mali: Kusafisha kiwandani, kwa mfano kutengeneza bustani. Hata hivyo, pole pole alianza kupiga picha kwenye maharusi na shughuli zingine zilizoandaliwa na Wamali kwa sababu alikuwa na ujuzi wa kutumia kamera.

24. O-Ton Daouda, French :

"Sote tulifanya kazi kinyume cha sheria. Tulifanya kazi za kuotea ambazo tulilipwa pesa taslimu, sio kwa hundi. Kila ukikutana na polisi ulikuwa unaogopa. Haikuwa rahisi hata kidogo. Shida zote hizo ndio zilinifanya nikarudi nyumbani."

25. Narrator:

Uamuzi huo pia haukuwa rahisi kwa sababu hakuwa na akiba ya kutosha. Daouda alizungumza na rafiki zake ambao walimshauri awasiliane na Shirika la Kimataifa linaloshughulikia maswala ya Uhamiaji. Huko alipata mafunzo ya usimamizi na shirika hilo lisilo la kiserikali lilimuahidi kumpa msaada mara atakapofika nyumbani. Mwaka 2006, kijana huyo alipanda ndege kurudi Mali. Miezi miwili baadaye, ofisi ya shirika la kimataifa linaloshughulikia maswala ya Uhamiaji ya mjini Bamako ikamnunulia kamera, kompyuta na vifaa vingine. Na hapo studio ya kutengeneza filamu ikazaliwa. Miaka miwili baadaye, Daouda ameridhika:

26. O-Ton Daouda, French :

"Ni sawa, ni sawa... ni bora kuliko kuwa mbioni, unawakimbia polisi wa Ulaya yote. Ninaendelea vizuri. Kichache ninachokipata si haba kwangu:"

27. Narrator:

Sasa kuna vifaa zaidi, studio hiyo ina kamera tatu na kompyuta nne. Huu ni ushahidi tosha kwamba biashara inaendelea vizuri. Na mkurugenzi ana mipango ya muda mrefu:

28. O-Ton Daouda, French :

"Nia yangu ni kuipanua studio yangu, kupata vifaa vipya, sio lazima kuwa na stesheni ya televisheni ila kuwa na vifaa vya hali ya juu."

29. Narrator:

Daouda, ambaye huwaajiri watu wawili hadi watano kutokana na kazi zilivyo, ameshatengeneza video pamoja na wanamuziki wa Mali na vipande hivyo vya muziki huonyeshwa kwenye televisheni ya taifa. Amepiga picha za video katika maharusi, siku za kuzaliwa na shughuli zingine kama hizo. Je. Anataka kurudi Ulaya?

30. O-Ton Daouda, French :

"Hapana, sio hasa (laughs), siwezi kusema kwamba sitakwenda kabisa, lakini nikienda itakuwa kwa matembezi tu. Lakini kama ni kwenda kufanya kazi, hapana asante!"

31. Narrator:

Kama Mamadou, muuza fanicha, Daouda anawataka wahamiaji wote kukumbuka nchi zao za uzawa:

32. O-Ton Daouda, French :

"Ushauri wangu kwa vijana wajasiri maisha ni kwamba warudi nyumbani waje wafanye chochote. Hayo ni maoni yangu lakini. Hayo ndio yaliyonifanya mimi nirudi Mali."

33. SFX : Music Fakoly

34. Narrator:

Baada ya kuwa Ulaya, Mamadou na Daouda wote wamefahamu kuwa inawezekana kupata mafanikio Afrika. Unachohitaji ni mawazo na ari ya kufanya kazi.

Outro:

Ni hayo tu kwa leo katika makala ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu Uhamiaji. Ripota wetu alikuwa Mahamadou Koné kutoka Mali. Asante kwa kutusikiliza. Iwapo ungependa kujifahamisha zaidi kuhusu kipindi hiki au kukisikiliza tena ama kusikiliza kipindi chochote katika makala ya Noa Bongo Jenga maisha Yako, tafadhali tembelea tovuti yetu. Anuani yetu ni: www.dw-world.de/lbe Kumbuka kusikiliza kipindi kifuatacho. Kwaheri.